

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
**CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU (FITI) – MOSHI**

**TANGAZO LA MAFUNZO**

**TANGAZO LA KUJIUNGA NA CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU KWA MWAKA WA MASOMO 2016/2017**

Mkuu wa Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) anatangaza nafasi za kujiunga na Chuo cha Viwanda vya Misitu kwa mwaka wa masomo 2016/2017. Chuo hiki kinapatikana mtaa wa Viwanda, wilaya ya Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro. Chuo hiki kinamilikiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, kimesajilwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa namba REG/ANE/019. Pia Mkuu wa Chuo anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa chuo kimefanya marekebisho makubwa ili kuhakikisha vijana wengi waliomaliza kidato cha nne na sita wanapata nafasi ya kujiunga na mafunzo ya Misitu, matumizi ya misitu na utunzaji wa mazingira kwa ujumla. Maboresho hayo ni kama ifuatavyo;

**1.** Ada za masomo zimeshuka sana ili kuwezesha vijana wengi kujiunga **2.** Chuo kinapokea maombi ya wanafunzi wa kutwa na bweni. **3.** Muundo wa ajira kwa vijana waliomaliza Chuo hiki sasa umetolewa na serikali ambao utakuwa unatumika katika sekta zote na taasisi nchi nzima hivyo kuongeza wigo wa kupata ajira kwa wahitimu.

**A. Mafunzo yanayotangazwa;**

**i. Astashahada (Cheti) ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu, NTA Level 4&5**

- Sifa za mwombaji:** - Awe amemaliza kidato cha nne  
- Awe amefaulu kwa alama D na kuendelea katika masomo mawili kati ya Fizikia, Kemia, Biolojia na Jiografia. Aidha mwombaji aliyefaulu katika masomo ya kiingereza au Hisabati atakuwa na nafasi kubwa ya kuchaguliwa kujiunga na mafunzo.

**Muda wa Kozi:** - Kozi hii ni ya muda wa miaka miwili (2)

**ii. Stashahada (Ordinary Diploma) ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu, NTA Level 6**

- Sifa za Mwombaji:** - Awe amemaliza kidato cha sita  
- Awe na "Principal pass" moja katika masomo ya michepuo ya sayansi au  
- Awe amemaliza kozi ya astashahada ya Viwanda vya Misitu au kozi zinazofanana na kozi hii
- Muda wa Kozi:** - Waombaji waliomaliza astashahada ya Viwanda vya Misitu watasoma kwa mwaka mmoja (1) tu.  
- Waombaji waliomaliza kidato cha sita na astashahada yoyote inayofanana na kozi hii watasoma kwa miaka miwili (2) tu.

**B. Ada ya Mafunzo na mahitaji mengine**

- i. Waombaji watakoachaguliwa watalipa ada ya sh. 800,000/= kwa mwaka.  
ii. Ada inaweza kulipwa kwa awamu mbili kwa mwaka  
iii. Waombaji watakoachaguliwa kujiunga na mafunzo watatakiwa kujilipia malazi, chakula na mahitaji mengine

**C. Jinsi ya kutuma maombi**

- i. Mwombaji anatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo atailipia sh 20,000/=  
ii. Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha Viwanda vya Misitu, kwenye tovuti ya chuo ([www.fiti.ac.tz](http://www.fiti.ac.tz)) na katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ([www.mnrt.go.tz](http://www.mnrt.go.tz))

**D. Tahadhari na Mwisho wa kutuma Maombi**

Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia taratibu za kujaza fomu, maombi yake hayatafikiriwa. Aidha mwombaji atakayebainika kugushi vyeti au hati nyingine atachukuliwa hatua za kisheria. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **30/05/2016**.

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo: **MKUU WA CHUO, CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU, S.L.P 1925, MOSHI.**

MKUU WA CHUO  
CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU  
Simu: 027-2755016  
Nukushi: 027-2753835  
Barua pepe: [info@fiti.ac.tz](mailto:info@fiti.ac.tz)